

- ix) Kamati itatoa hukumu juu ya malalamiko ikiamuru hatua kuchukuliwa na idara ama kitengo husika.
- x) Kamati kwa kuzingatia kipengele cha 41 cha sheria ya udhibiti wa huduma za maji na nishati ya mwaka 2001 itatoa agizo kwa mtoa huduma kufanya yafuatayo:-
- Kutoa huduma husika kwa muda utakaoamriwa.
 - Kutoa huduma kwa kufuata masharti na taratibu zitakazoamriwa.
 - Kulipa gharama za upande mwingine kwa ajili ya kuhudhuria kwenye kusikiza shauri ama kwa kutengeneza makabrasha.
 - Kuachana na shauri.
 - Kutozwa faini kulingana na kesi yenyewe.
 - kufanyika maamuzi mengine ya namna yoyote ile kama itakavyoonekana yanahitajika.
- xi) Pale ambapo upande mmoja hautaridhika na hukumu iliyotolewa na Kamati, upande huo unaweza kukata rufaa kwenda kwenye Tume ya Ushindani pekee ndani ya siku 21.
- xii) Mwathirika wa hukumu atatakiwa kukata rufaa kwa misingi tu ifuatayo:-
- Hukumu haikuwa na uthibitisho wa kutosha.
 - Hapakuwa na mapungufu ya kisheria.
 - Taratibu ama mahitaji mengine ya kisheria hayakuendana na kanuni zilizopo.

- Mdhibiti hakuwa na mamlaka ya kisheria kufanya maamuzi ama kutoa hukumu.
- xiii) Tume ya Ushindani baada ya kusikiliza rufaa inaweza kufanya yafuatayo:-
- Kuachana na rufaa kwa ujumla wake ama baadhi ya vipengele vilivyoainishwa
 - Kuweka pembeni hukumu yote au baadhi ya vipengele vya hukumu husika na kumrejeshwa mdhibiti kipengele kinachoonekana kuwa na uzito mkubwa kwa ajili ya kukishughulika upya.
 - Mwathirika wa hukumu kama hatakuwa ameridhika na hukumu iliyotolewa baada ya kufuata ngazi zote zilizoainishwa, anaweza kuiomba Kamati ya Ndani ya Kurejea Maamuzi (Internal Review Committee) kufanya hivyo ndani ya siku 14.

JE UNA MAONI AU USHAURI?

Wasiliana nasi kupitia anuani ifuatayo:-

Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za EWURA.

Jengo la INFOTECH Place, Ghorofa ya pili, Kushoto, Barabara ya zamani ya Bagamoyo, Mikochoeni/Kawe.

P.O. Box 72175, Dar es Salaam, Tanzania.

TEL: (+255-22) 2780236; FAX: (+255-22) 2780238

Barua pepe: info@ewuracc.go.tz

Wavuti: www.ewuracc.go.tz



BARAZA LA USHAURI LA WATUMIAJI WA HUDUMA ZA MAJI NA



MCHAKATO WA KUWASILISHA NA KUSHUGHULIKIA MALALAMIKO YA MTUMIAJI